



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA NYASA



*Unapojibu tafadhali taja!*

Kumb.Na:NDC/I.20/2

02 Februari, 2023

### TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

- 1.1 Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa ni chombo kilichoundwa kisheria kwa mujibu wa aya ya 145 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Aidha, kwa mujibu wa tangazo la Serikali Na. 11 Vol 95 la tarehe 14 Machi, 2014 likisomwa pamoja na Marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 18/2007, Halmashauri mbali na kuwa na majukumu mengine, inalo jukumu la kuajiri watumishi wa kada mbalimbali za Halmashauri
- 1.2 Hivyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa anawatangazia Watanzania wenye sifa zilizoainishwa hapa chini na ambao wapo tayari kufanya kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa kuleta maombi yao ya kazi. Nafasi hiyo ni kwa Watanzania wote.

#### 2.0 Mtendaji wa Kijiji III (Village Executive III) TGS B<sub>1</sub> – NAFASI 1

##### *Sifa za Kuingilia*

1. Kuajiriwa mwenye kidato cha IV au VI aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/cheti katika moja ya fani zifuatazo; Utawala, sheria, Usimamizi wa Fedha, Elimu ya Jamii, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Jamii kutoka chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo – Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali

## 2.1 Kazi za Mtendaji wa Kijiji

1. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Kijiji
2. Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa Mipango ya maendeleo ya Kijiji
3. Kutafsiri na kusimamia será, taratibu na Sheria
4. Kusimamia ulinzi na usalama wa raia na mali zao, kuwa mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji
5. Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali,
6. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji.
7. Katibu wa Mikutano ya Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji, na
8. Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya Wananchi.

## 3.0 Utaratibu wa Kutuma maombi

Waombaji wote wanatakiwa kutuma maombi yao kwa Mkurugenzi Mtendaji kwa Anuani iliyooneshwa hapo chini kwa utaratibu ufuatao;-

1. Mwombaji sharti awe ni raia wa Tanzania, awe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45
2. Barua ya maombi iliyoandikwa kwa mkono inayoonesha nafasi inayoombwa na Namba ya simu ya Mwombaji.
3. Nakala za vyeti vya Elimu (cheti cha matokeo kidato cha IV, Kidato cha VI
4. Nakala ya vyeti vya kuhitimu mafunzo ya fani walizosomea
5. Picha 01 za Rangi "Passport size" ya hivi karibuni
6. Nakala ya cheti cha kuzaliwa
7. Nakala ya hati ya maelezo binafsi (Curriculum Vitae/Resume) yenye taarifa za anuani na namba za simu za kuaminika na majina ya wadhamini watatu (Referees) wa kuaminika na namba zao za simu.

## 3.0 Maombi yote yatumwe kwa njia ya Posta au kwa kuletwa ofisini;

Mkurugenzi Mtendaji (W),  
Halmashauri ya Wilaya,  
S.L.P 90,  
Nyasa – Ruvuma  
Tanzania.

Tangazo hili linapatikana pia katika wavuti ya Halmashauri, ([www.nyasadc.go.tz](http://www.nyasadc.go.tz))  
Na wavuti ya Serikali ya Ajira katika Utumishi wa Umma

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 23 Siku ya Alhamisi Saa 9-30

Jimson P. Mhagama  
MKURUGENZI MTENDAJI (W)

